



## **BENKI YA WATU WA ZANZIBAR LTD (PBZ) TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

### **UTANGULIZI**

Benki ya Watu wa Zanzibar Limited (PBZ) ni benki ya kibiashara inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100%. Benki inaendelea kutoa huduma bora za kifedha kwa wateja wake Zanzibar na Tanzania Bara.

Katika jitihada zake za kuimarisha utoaji wa huduma bora na kukuza/kuongeza mauzo ya bidhaa zake, PBZ inakaribisha maombi kutoka kwa vijana wenye ari, ubunifu na uwezo mzuri wa kushawishi wajiunge na Benki kwa nafasi ya **Mauzo (Sales)** katika Idara ya Masoko. Ajira hizi zitakuwa kwa mkataba wa muda maalum.

### **NAFASI: Afisa Mauzo (Sales Officer) - Nafasi 24**

#### **MAENEO YA KAZI:**

Matawi na vituo mbalimbali vya PBZ vilivyopo Tanzania Bara kama ifuatavyo:-

1. Dar es Salaam – Nafasi 6,
2. Mtwara – Nafasi 3,
3. Dodoma-Nafasi 3,
4. Mbeya- Nafasi 3
5. Mwanza-Nafasi 3,
6. Arusha- Nafasi 3,
7. Morogoro-Nafasi 3

#### **MAJUKUMU YA KAZI:**

- Kutangaza na kuuza bidhaa na huduma za Benki kwa wateja wapya na waliopo.
- Kuwahamasisha wateja kufungua akaunti na kutumia bidhaa za Benki.
- Kutoa maelezo sahihi kwa wateja kuhusu huduma za PBZ na kuhakikisha wateja wanaridhika.
- Kuhusika na shughuli zote za mauzo na masoko.
- Kufikia malengo ya mauzo yaliyowekwa na kuwasilisha taarifa za utendaji kwa wakati.



#### **SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Awe Mtanzania
- Mwenye umri usiozidi miaka 35.
- Awe na Shahada katika fani za Masoko, Biashara, Uhasibu, Uchumi, Benki, Bima, Mahusiano wa kimataifa au fani inayofanana na hizo.
- Awe na CV na Cheti cha kuzaliwa.
- Awe na uwezo mzuri wa kuwasiliana na kushirikiana na watu.
- Awe na ari ya kazi, mshawishi, na mwenye lengo la kufikia matokeo.
- Awe tayari kufanya kazi kwa kujitegemea katika mazingira yenye changamoto.
- Awe na vyeti halisi vya kumalizia masomo.
- Awe si muajiriwa wa Serikali.

#### **UWEZO NA SIFA BINAFSI (COMPETENCIES):**

- Ubunifu na uwezo wa kutatua changamoto kazini.
- Kujituma na kuwa na shauku ya kuuza na kuhudumia wateja.
- Nidhamu, uwajibikaji, na uaminifu kazini.

#### **JINSI YA KUOMBA:**

Maombi yote yawasiliswe kwa njia ya kielektroniki kwenye mfumo wa maombi ya ajira kupitia anuani ifuatayo:

**[Bonyeza hapa](#) kuanzia tarehe 13 Aprili 2026 hadi tarehe 17 Aprili 2026.**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya PBZ ambayo ni [www.pbzbank.co.tz](http://www.pbzbank.co.tz)

Barua za maombi zianishe anuani ifuatayo:

**MKURUGENZI MWEENDESHAJI,  
BENKI YA WATU WA ZANZIBAR,  
ZANZIBAR.**

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha:

- **Barua ya maombi ya kazi,**



- **Wasifu binafsi (CV),**
- **Nakala za vyeti vya taaluma,** na
- **Nakala ya Cheti cha kuzaliwa.**
- **Nakala ya Vitambulisho vya Taifa (ZANID/NIDA)**

Aidha, muombaji anatakiwa kuanisha nafasi ya kazi anayoiomba na *inashauriwa* muhusika awe mwenyeji wa eneo analo omba kazi.

- a. Muombaji atakaewasilisha **“Progressive Report”** au **“Statement of Result”** maombi yake hayatozingatiwa.
- b. Muombaji haruhusiwi kuomba zaidi ya nafasi moja.

Ahsante,